# HATI YA MAELEZO: KUJUA KUHUSU GLOBAL NETWORK INITIATIVE (GNI)

- GNI ilizinduliwa mwezi Oktoba 2008, kufuatia miaka miwili ya mazungumzo na majadiliano miongoni kwa washikadau tofauti.
- GNI ni muungano wa zaidi ya kampuni 60 za teknolojia ya maelezo na mawasiliano (ICT) , mashirika ya jamii za umma (CSOs) (pamoja na makundi ya haki za binadamu na uhuru wa wanahabari), wawekezaji, na wasomi.
- GNI ina makao makuu mjini Washington, D.C., na Amsterdam, na ina wanatimu walio mjini New York City.

## MISHENI

Misheni ya Global Network Initiative ni kulinda na kuruhusu haki za uhuru wa kujieleza na faragha katika sekta ya ICT kwa kuweka kiwango cha kiulimwengu cha kampuni kufanya maamuzi ya busara na kuhudumu kama sauti ya washikadau wengi wakati wa vikwazo na mahitaji ya serikali.

GNI inatekeleza misheni yake kupitia nguzo za kimkakati chini ya uelekezi na operesheni za mfumo wake wa utawala. Nguzo za kimkakati ni:

1. Kutoa mfumo wa kufanya maamuzi ya busara
2. Kukuza uwajibikaji ili kuleta uaminifu
3. Kutekeleza sera ili kukuza haki za kibinadamu
4. Kuwezesha mafunzo ili kutengeneza mazoea bora

## UTAWALA

Hati ya Utawala ya GNI inabainisha majukumu na wajibu wa washiriki. Mkurugenzi Mtendaji wa GNI na wafanyakazi wachache wanadhibiti shughuli za kila siku za GNI na Mwenyeketi Huru anaongoza Bodi ya Wakurugenzi inayojumuisha idadi sawa ya wawakilishi wa kampuni na wasio wa kampuni. GNI imesajiliwa kama shiriki lisilo la kifaida chini ya sheria za Marekani

## WANACHAMA

Wanachama wanaoongezeka wa GNI wanajumuisha kampuni za ICT, mashirika ya jamii za umma, wasomi na taasisi za masomo, na wawekezaji kutoka barani Afrika, Asia, Ulaya, Amerika Kusini, Amerika Kaskazini, na Mashariki ya Kati.

Wanachama wote wanashiriki jitihada kwenye Kanuni za GNI na hati kuu za GNI, huku wakichangia katika mafunzo ya pamoja, na hatua za pamoja miongoni mwa washiriki wa GNI.

## VIUNGO

- Jitihada Kuu
  - Kanuni za GNI
  - Miongozo ya Utekelezaji
  - Uwajibikaji, Sera, na Mfumo wa Mafunzo
  - Hati ya Utawala
- Bodi ya Wakurugenzi
- Orodha ya Wanachama
- Tathmini za Kampuni
  - Zana za Tathmini
  - Ripoti ya Tathmini ya Umma ya 2018/19
- Ripoti za Mwaka
- Maadhimisho ya Miaka Kumi ya GNI
- Jisajili kupokea Mipasho ya Kila Robo Mwaka kupitia Barua Pepe

GLOBAL NETWORK INITIATIVE

# JITIHADA KUU NA MFUMO

- Kanuni za GNI zinaangazia jitihada kubwa ya wanachama ya kushirikiana katika ukuzaji haki za watumiaji za uhuru wa kujieleza na faragha. Kanuni hii zinatoa mwongozo wa hali ya juu kwenye sekta ya ICT kuhusu jinsi ya kuheshimu, kulinda, na kukuza haki za watumiaji za uhuru wa kujieleza na faragha, pamoja na wakati inakumbwa na mahitaji ya serikali ya udhibiti na ufichuaji wa maelezo ya kibinafsi ya mtumiaji.

- Miongozo ya Utekelezaji inatoa mwongozo wa kina zaidi kwa kampuni ya ICT kuhusu jinsi ya kutekeleza Kanuni, na pia kutoa mfumo wa ushirikiano miongoni mwa kampuni, CSOs, wawekezaji, na wasomi.

- Kanuni na Miongozo ya Utekelezaji ina msingi kwenye sheria ya kimataifa ya haki za binadamu na kuambatana na Kanuni Zinazoongoza Biashara na Haki za Binadamu za Umoja wa Mataifa (United Nations Guiding Principles on Business and Human Rights (UNGPs)).

## UWAJIBIKAJI

Kampuni zinawajibika kupitia mfumo wa tathmini inayofanywa na mhusika mwingine ili kutathmini jinsi kampuni inavyoambatana na Kanuni na Miongozo ya Utekelezaji. Kampuni zinatarajiwa kuonyesha nia nzuri ya kutekeleza Kanuni na Miongozo hiyo, na kuboresha baada ya muda.

Mchakato wa tathmini unafanyika kila baada ya miaka miwili. Kulikuwa na chelewa chelewa kati ya tathmini za kipindi cha 2015/16 na 2018/19 kwa ajili ya mchakato wa kuhakiki mbinu ya tathmini, kutengeneza Zana ya Tathmini na kupanga tathmini kwa ajili ya idadi iliyoongezeka ya kampuni ambazo ni wanachama

## SERA

Tunatumia sauti ya kipekee na ya mshikadau nyingi ya GNI kwenye vipaumbele vya sera ambavyo wanachama wetu wametambua, pamoja na udhibiti wa maudhui, ufuatiliaji, na udakizaji wa mtandao. Tunatoa kauli, kutoa maoni kuhusu mapendekezo husika ya kiudhibiti, kuwahusisha watengenezaji sera, na kushiriki katika miradi ya kiulimwengu kama vile Freedom Online Coalition na Christchurch Call ili kuboresha vipaumbele hivyo.

## MAFUNZO

GNI mara kwa mara inaletea wanachama fursa za kushiriki ujuzi wao na kukuza mafunzo ya faraghani kwenye masuala ya teknolojia mpya, mazoea mazuri ya kibiashara, na hali zenye changamoto.

***GNI inachapisha ripoti ya mwaka ya shughuli zake na ripoti ya tathmini ya umma baada ya kukamilisha mchakato wake wa tathmini ya kimsimu. GNI pia inachapisha kauli na machapisho mengine kwenye tovuti yake na pia kutoa jarida la robo mwaka kupitia barua pepe. Unaweza kufuatilia GNI kwenye mitandao ya kijamii kwenye Facebook, LinkedIn, na Twitter.***

718 7th Street, NW, Suite 200 Washington, DC 20001

www.GlobalNetworkInitiative.org | info@GlobalNetworkInitiative.org

GLOBAL NETWORK INITIATIVE